**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Mkuu wa Shule 0782586468/0717402768**

**M/Mkuu wa Shule 0684971079/0682825963**

**Matron 0782203484**

**Shule ya Sekondari ilulu**

**S.L.P. 139 kilwa masoko**

**12-06-2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI ILULU ILIYOPO HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA MKOA WA LINDI MWAKA 2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari Ilulu ipo umbali wa mita mia tatu (300) kutoka kituo cha basi cha kijiji cha Njia nne kuelekea Mashariki mwa kijiji cha Njia nne. Unaweza kufika shuleni kwa kutokea Dar –es Salaam kwa kutumia usafiri wa basi kutoka katika kituo cha Mabasi Mbezi/Mbagala Rangi Tatu utashuka kijiji cha Njia nne.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **14/08/2023**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **13/08/2023** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/08/2023.**

Pamoja na barua hii, pokea,

a) Fomu ya kupimwa afya ya mwanafunzi;

b) Fomu ya Taarifa za ndugu wa karibu;

c) Fomu ya ahadi ya kutekeleza wajibu.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

(i) Mwanafunzi aje na sketi mbili za damu ya mzee (maroon) kitambaa kizito. Sketi zake ziwe ndefu kutoka kwenye kisigino mpaka kwenye pindo la sketi zisizidi sentimita 18 au inchi $7^{1}/_{2}$. Zingatia vipimo. Sketi zake ziwe na (belt) mkanda, upana wa belt usizidi sentimeta 5 au inchi moja na nusu. Mshono wa sketi ni linda box (Linda kubwa mbele na nyuma). Tazama mfano wa picha hapo chini.

(ii) Mzazi/mlezi na mwanafunzi tafadhali zingatia vipimo hivyo, mwanafunzi atakayeshona na kuja na sketi/shamba dress kinyume na vipimo, rangi na aina ya kitambaa tulichoelekeza hatapokelewa,;

(iii) Mwanafunzi anaweza kushona idadi ya sare kadri ya uwezo wake. Ila inashauriwa awe na angalau sare za darasani mbili na gauni za kazi mbili.

(i) Shati (blauzi) nyeupe mbili (2) au zaidi mikono mifupi tetroni — Tomato;

(ii) Soksi nyeupe jozi mbili (2) au zaidi;

- Hijabu ya tetroni nyeupe ya kitamba aina ya halua na sio mtandio,
- Hijab isiwe na urembo wowote ikiwemo lessi

iii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye gidamu (kamba) (Visiwe na Visigino Virefu) jozi mbili;

iv. Jezi (bukta na t-shirt) nyeusi kwa ajili ya michezo;

v. Raba nyeupe kwa ajili ya michezo;

vi. Track Suit nyeusi isiyobana, isiyokuwa na maandishi na yenye mistari meupe kwa ajili ya maandalizi ya jioni.;

vii. Gauni la kazi za nje la kitambaa kizito (shamba dress) rangi ya blue ya bendera ya taifa mshono wa solo ya kuunga, kama anavaa hijabu ashone rangi ya blue.

viii. Aje na T-shirt rangi ya njano yenye kola ya ufito mweusi na njano, utagongewa nembo kwa Tsh 4000/= Tsheti zinapatikana shuleni kwa ghrama ya Tsh. 14000/= pamoja na nembo ya shule

ix. Sweta rangi ya damu ya mzee lenye nembo ya shule kwa anayehitaji linapatikana shuleni kwa Tsh 15,000/= au uje na sweta lenye muundo wa V mbele na utagongewa nembo kwa Tsh 2000/=

**NB:** Fedha ya T- shirt na sweta iletwe mkononi (cash) isiingizwe bank

**MUHIMU:** Sare ya shule ni kama ilivyoelekezwa hapo juu. Kila Mwanafunzi atavaa sare wakati wote wa masomo, na anapokwenda hospitali, mjini au anapokuwa katika shughuli za kishule nje ya eneo la shule. Ni marufuku ujipamba wakati amevaa sare ya shule. Aidha, lipo vazi la kazi za nje ambalo huvaliwa na wanafunzi wanapokuwa katika kazi za mikono nje ya masomo.

## 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo:-

i. Aje na sanduku (sanduku la bati) linalofunga vizuri kwa kuhifadhia nguo na vitu vyake.

ii. Aje na godoro futi $2^{1/2}$ x 6

iii. Aje na vifaa vya usafi binafsi kama mswaki, sabuni n.k

iv. Aje na Mto na Foronya yake ya bluu bahari kwa anayetumia

v. Shuka za kulalia jozi (pair) mbili za futi 3x6 (rangi ya bluu bahari isiwe na maua)

vi. Taulo moja(1) au mbili (2)

vii. Nguo za ndani za kutosha;

viii. Kandambili kwa ajili ya kuogea.

ix. Viatu vya plastiki chipsi rangi yoyote - vya kushindia

x. Ndoo ndogo mbili (matumizi yake binafsi bwenini)

xi. Alete container lenye mfuniko/ sahani, bakuli, kikombe na kijiko (vyombo vya chakula)

xii. daftari ( kaunta books) quire three kumi (10)

xiii. Mathematical set moja (1) kwa matumizi yake awapo darasani

xiv. Vitabu vya ibada kwa mujbu wa dhehebu lake

xv. Leta nakala halisi ya result slip ya kidato cha nne;

xvi. Leta nakala (kopi)ya cheti cha kuzaliwa;

xvii. Alete na neti nyeupe ya kitanda cha futi 3x6;

xviii. Dissecting kit (kwa wanaosoma Biology;

xix. Koti la maabara jeupe (wote kwa wanaosoma sayansi)

xx. Kwa wanafunzi watakaosoma BAM ni vizuri wanunue Scientific Calculator Graph pad moja (1) kwa wanaosoma geography na masomo ya sayansi;

xxi. Mwanafunzi aje na Bima ya Afya, kama hana mzazi aandae utaratibu wa kupata bima ya Afya akiwa shuleni.

**VIFAA VYA USAFI**

i. Soft broom moja (fagio laini la ndani;
ii. Hard broom moja (fagio gumu la ndani;
iii. Drier moja (mopa);
iv. Dawa ya chooni lita 2. Au uje na Tsh 4,000/= utapata lita 2 shuleni;
v. Pia aje na vifuatavyo kulingana na tahasusi yake kwa ajili ya usafi

- HGL — Panga na Brashi ngumu yenye mpini mfupi wa mbao/mti moja kwa ajili ya kusafishia sinki la choo. Asilete yenye mpini wa plastic
- HKL — Fyekeo na ufagio wa chelewa ya wima
- CBG & HGK —Jembe lenye mpini

**MUHIMU: Mwanafunzi alete kifaa na sio pesa.**

**Nguo nyingine**

i. Aje na nguo za ndani pamoja na khanga au kitenge doti moja tu.
ii. Mwanafunzi aje akiwa amevaa sare za shule,
iii. Mwanafunzi anaruhusiwa kuvaa Track Suit wakati wa maandalio ya jioni. Kinyume na hapo atarudishwa nyumbani kurejesha nguo zisizotakiwa kwa gharama zake.
iv. Mwanafunzi anaweza kuja na nguo za kulalia (night dress)

## 2.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| **Jumla** | | **80,000/=** |

*Michango yote itumwe kwenye akaunti ya shule NAMBA **70103200012** Benki ya NMB (Ilulu Secondary School-Development account) na mwanafunzi afike na risiti halisi ya Benki..*

**b) Ream mbili (02) za karatasi kwa mwaka, moja ya Photocopy A4 na moja ya mistari (rulled)**

**NB:** Vifaa vyote vya usafi, darasani, dawa ya chooni na godoro vinapatikana katika Maduka na Stationery za karibu, unaweza ukaleta au ukaja kununua huku.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
**ii. Mwanafunzi anatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote awapo shuleni.**
iii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iv. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
v. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
vi. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vii. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
viii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
ix. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
x. Kutunza mali za shule;
xi. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xii. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kunyoa nywele kwa mtindo wowote ule(panki, kisahani, kiduku n.k). Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………………….**

**Jina la Mkuu wa Shule AMINA S MANDALI**

THE HEADMISTRESS
ILULU SEC. SCHOOL
P. O. Box 139
KILWA - MASOKO

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa**.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule -0717402768 au 0782586468**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0682825963 au 0684971079**
- **Mwandamizi Taaluma 0788393774**
- **Mwandamizi Malezi 0786790947**

**NB: MWANAFUNZI HATOPOKELEWA IKIWA ATARIPOTI BILA KUJAZA FOMU ZILIZOAMBATANISHWA**

**KUKUBALI AU KUKATAA NAFASI YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KWA MWAKA 2023.**

Mimi ………………………………………………………… nakutaarifu kuwa nimepokea barua ya kuchaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Ilulu. NIMEKUBALI/ NIMEKATAA nafasi hii baada ya kusoma na kuelewa yaliyoandikwa katika fomu na barua ya kujiunga.

Ninaahidi mbele ya Mzazi/Mlezi wangu kuwa nikishafika shuleni, nitazingatia kanuni, sheria na taratibu zote za shule kwa kipindi chote cha mimi kuwa mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Ilulu. Na nimeelewa kanuni na taratibu zote za shule na sitajihusisha na vitendo vya uvunjaji wa amani shuleni, kushiriki kufanya fujo, vurugu, migomo, kuvuta bangi na matumizi ya madawa ya kulevya pamoja na makosa ya jinai.

Nitatumia juhudi na maarifa katika kujiendeleza kwa manufaa yangu na Taifa kwa ujumla.

Jina la mwanafunzi ……………………………………………… Saini…………………….

Tarehe……………………………..….

**FOMU NAMBA 1.**

To the Medical Officer

………………………………………………………………………….…..

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION TO …….……………………………………….

Please examine the above named pupil and give us the report regarding his/her suitability for undertaking secondary school students.

1. Blood
2. Stool ………………………………………………………………………………………...
3. T.B. Test……………………………………………………………………………….
4. Syphilis Test…………………………………………………………………………………...
5. Urine Examination …………………………………………………………………………..
6. Eye Test ……………………………………………………………………………….
7. Chest Test ……………………………………………………………………………...
8. Ears Test ……………………………………………………………………………………..
9. Spleen …………………………………………………………………………………………..
10. Abdomen ……………………………………………………………………………………
11. Pregnancy……………………………………………………………………………………

ANY ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical defects or impairment, infection, family diseases etc.

……………………………………………………………………………………………

I certify that, the above pupil is suitable/unsuitable for secondary school students. If unsuitable give reasons:

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………

Name of Medical Officer: ……………………………………Signature ……………………… Date:

………………………………        Official stamp ………………………………

**FOMU NAMBA 2.**

TAARIFA ZA ANAKOTOKA MWANAFUNZI

1. Mkoa …………………..……………………… Wilaya ………………………….……………
2. Tarafa ……………………………….…………. Kata ………………………….……….……
3. Mtaa/Kijiji ………………………….………………
4. Jina la Mtendaji wa Kijiji/Mtaa ……………………………..………….Saini………………….

   Tarehe……………………………… Mhuri…………….……………… Simu…………………...

5. **Michezo anayopendelea**

| **Na** | **Jina la Mchezo** |
|---|---|
| 1 | |
| 2 | |
| 3 | |
| 4 | |
| 5 | |

9. **Nafasi yoyote ya uongozi aliyowahi kushika**

| **Na.** | **Aina ya uongozi** | **Shule** | **Mwaka** |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

Nathibitisha kwamba taarifa nilizozitoa hapo juu ni za kweli, pia nathibitisha kuwa nitakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi pamoja na kuwa na bidii ya masomo

NB: Pamoja na fomu hizi ambatanisha na kopi ya cheti cha kuzaliwa na nakala halisi ya matokeo.

Jina la Mwanafunzi …………………………..Saini ………………… Tarehe ……………

**FOMU NAMBA 3.**

TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI

1. Jina kamili la Mzazi/Mlezi …………………………………………………………………….

2. Kazi ………………………………………………………………………………………...

3. Anuani ………………………………………… Namba ya simu ……………………………….

4. Mkoa ………………………… Wilaya ……………………….. Tarafa ………….………………

5. Kata ……………………………………Mtaa/Kijiji ……………………………………………

6. **Ndugu wa karibu wa mwanafunzi**

| Na. | JINA | UHUSIANO | ANAPOISHI | SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |

Mimi Mzazi/Mlezi wa ……………………………………………………………… ninaahidi kushirikiana na walimu pamoja na watumishi wote wa Shule ya Sekondari Ilulu katika kumlea mwanangu kwa muda wote atakapokuwa shuleni.

Nitaomba kujulishwa mara moja endapo mwanangu ameenda kinyume na sheria, kanuni na taratibu za shule. Pia nitakuwa tayari mwanangu kupewa adhabu inayostahili kwa makosa atakayofanya.

Jina la Mzazi/Mlezi ……………………………Saini …………………Tarehe ……………….

## ORODHA YA VITABU MUHIMU VYA KUJA NAVYO SHULENI

### GENERAL STUDIES

1. Understanding General Studies for advanced level. JOANNES BIGIRWAMUNGU
2. General Studies alive — ZISTI KAMILI

### HISTORY 1

1. Lesson Notes for Advanced History Paper 1-Bakari Madaya

### HISTORY 2

1. Contemporary historical events — volume 2 by shibitali C. K
2. Essentials in Advanced level History — book 2 by saleh Yassin
3. Mastering Advanced level History — book 2 by Abubakar kato
4. Advanced level history — part two alive by Zisti Kamili

### KISWAHILI 1

1. Kiswahili 1 kidato cha 5 na 6 (TIE)
2. Nadharia ya lugha - Nyambari na Masebo

### KISWAHILI 2

1. Nadharia ya fasihi Kiswahili 2 kidato cha 5 na 6;
2. Kiswahili 2 (Tahakiki ya Kiswahili) shule za sekondari, kidato cha 5 na 6.

### ENGLISH 1

1. Nicholaus Asheri: Advanced level English;
2. Francis Mnyawi: Contemporary English for Advanced level
3. Kadeghe Michael: Advanced level English form 5
4. Oxford Advanced level English form 5 & 6

### ENGLISH 2

1. Nicholaus Asheri: Advanced level English Literature
2. Nyambari Nyangwine: Advanced level English Literature
3. Francis Mnyawi: Advanced level English Literature

**GEOGRAPHY 1**

1. Physical geography — Zisto Kamili (2016
2. Physical geography intergrated Aproach — by David Waugh

**GEOGRAPHY 2**

1. HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY PAPER 2 BY MSABILA DT

**CHEMISTRY 1**

1. Conceptual Chemistry for class xi: Dr. S.K Jain
2. Hopegen book project (HBP) Physical chemistry (NGAIZA SERIES)

**CHEMISTRY 2**

1. Hopegen book project (HBP) (ORGANIC CHEMISTRY (NGAIZA, LUSIMA
2. Chemistry for secondary school form five (TIE)

**BAM**

1. Basic Applied Mathematics for Advanced level secondary schools: By Tanzania Institute of Education (T.I.E), (2019)

**BIOLOGY 1**

1. Biology foe advanced leveal secondary school
2. Students book form five — Tanzania institute of education (TIE, 2019)
3. Dissecting kit

**BIOLOGY 2**

1. Biology foe advanced leveal secondary school
2. Students book form five — Tanzania institute of education (TIE, 20

MFANO WA RANGI YA SARE NA AINA ZA MISHONO

Shamba dress



sketi ya shule yenye mshono wa linda box

